



## TAARIFA ZA BAADHIYA MIRADIYA BARABARA INAYOTEKELEZWA NA TARURA WILAYA YA GAIRO - MKOA WA MOROGORO

### MKAKATI WA CoST

Mkakati wa CoST, unaotekelezwa chini ya uangalizi wa Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), unalenga kuongeza Uwazi na Uwajibikaji katika utekelezaji wa miundombinu ya umma ili utekelezaji wake ulingane na thamani ya fedha zinazotumika. Mkakati huu unashirikisha sekta zote kuu tatu – Umma, Binafsi na Asasi za Kiraia (CSOs).

Majukumu makuu ya CoST ni:

- Kuhamasisha Taasisi Nunuzi za Umma kutoa taarifa za utekelezaji wa miradi ya miundombinu ili kujengea umma uelewa wa miradi hiyo;
- Kutoa taarifa za utekelezaji wa miradi ya Miundo Mbinu kwa umma;
- Kuhakiki taarifa za utekelezaji wa miradi ya miundombinu (assurance);
- Kuhamasisha na kuwahusisha wadau wote katika ufuatiliaji wa uwazi na uwajibikaji katika miradi ya sekta ya ujenzi;
- Kubuni mikakati mbalimbali ya kuwajengea uwezo wadau mbalimbali ili washiriki katika shughuli za uongezaji wa uwazi na uwajibikaji katika miradi ya ujenzi kwa ufanisi wa kutosha.
- Kufuatilia na kushauri juu ya uboreshaji wa sera na sheria mbalimbali zinazohusu uwazi na uwajibikaji.

### TARURA

Katika awamu hii ya utoaji taarifa, CoST Tanzania inashirikiana na Wakala wa Barabara mijini na Vijijini (TARURA) kutoa taarifa za miradi inayotekelezwa katika wilaya za Gairo, Kilosa, Morogoro Vijijini katika Mkoa wa Morogoro na Chamwino, Kongwa na Mpwapwa katika Mkoa wa Dodoma.



### LENGO LA KUTOA TAARIFA KWA UMMA

Lengo la kutoa taarifa hizi kwa umma, na hasa kwa vijiji vinavyopitiwa na barabara husika ni:

- Kuwafahamisha wahusika juu ya miradi hiyo ili wajitayarisha kutoa ushirikiano na kujenga mahusiano na TARURA;
- Kuhamasisha wahusika kutoa taarifa zitakazofanikisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa ufanisi na kwa gharama stahiki zikibainisha, kwa mfano maeneo yafuatayo:

- Sehemu ambazo kihistoria zimekuwa na usumbufu;
- Uwezekano wa kuwa na makinzano na haki na mategemeo ya wananchi ;
- Chanzo cha mali ghafi hasa kifusi, changarawe, maji, n.k.;
- Mambo yahasuyo mazingira;
- Haki ya kutumia ardhi inakopita barabara;
- Chanzo cha nguvu kazi; na
- Ufuatiliaji wa jumla wa miradi ili kuhakikisha inajengwa kwa thamani stahiki na kuhakikisha umma unapata kilicho bora; n.k.

### MAWASILIANO

Toa taarifa zako kwa Mtendaji Kijiji, Mtendaji Kata, au CoST kwa kutumia mawasiliano yaliyoko hapo chini.

**TAARIFA ZA MIRADI YA BARABARA INAYOTEKELEZWA NA TARURA JULAI - SEPTEMBER 2018  
WILAYA YA GAIRO (MAKISIO YANAJUMLISHA KAZI, USIMAMIZI NA UTAWALA)**

Road Code	JINA LA BARABARA	JINA LA KATA	VIJJI	Tenda No. AE/092/2018-2019/ MOR/ ...	FUNGU	TAREHE YA KUTANGAZWA TENDA	TAREHE YA KUFUNGA TENDA	KUTAARIFIWA MKANDARASI	MAKISIO YA JUMLA TZS MI.
Matengenezo ya kawaida, Matengenezo ya muda maalum na marekebisho ya sehemu korofi za barabara ya Nongwe - Unonesala na Matengenezo ya kawaida ya barabara ya Chagongwe - Lufikiri - Kumbulu									
57036	Nongwe - Unonesala	Nongwe	Nongwe, Mtega, Uhone	W/28	I	24/7/2018	6/8/2018	17/9/2018	100.34
57053	Chagongwe - Lufikiri - Kumbulu	Chagongwe	Chagongwe, Lufikiri, Kumbulu						
Ujenzi wa daraja kwenye barabara ya Mlebule-Chanjale na Marekebisho ya sehemu korofi kwenye barabara ya Chingholwe - Mwenzele (No.30) - Manvisi.									
57045	Mlebule-Chanjale	Chanajale	Ching'olwe, Chanjale, Kumbulu						
57044	Chingholwe - Mwenzele (No.30) - Manvisi.	Chanajale	Ching'olwe, Kumbulu, Manvisi	W/29	I	24/7/2018	6/8/2018	17/9/2018	91.5
Matengenezo ya kawaida ya barabara ya Rubeho-Kisitwi na Matengenezo ya Kawaida, Matengenezo ya muda maalum kwa barabara ya Rubeho - Kishambo-Mamiwa pamoja na Matengenezo ya kawaida, Marekebisho ya sehemu korofi kwenye barabara ya Mandege - Ngege									
57049	Rubeho-Kisitwi,	Rubeho	Rubeho, Kisiwi						
57090	Rubeho - Kishambo-Mamiwa	Rubeho	Rubeho, Kishambo, Mamiwa						
57043	Mandege - Ngege	Mandege	Mandege, Njugwa	W/30	I	24/7/2018	6/8/2018	17/9/2018	74.88
Matengenezo ya kawaida ya barabara ya Chakwale-Leshata, & Marekebisho ya sehemu korofi, Matengenezo ya muda maalum na ujenzi wa kalavati kwenye barabara ya Leshata Idibo & Matengenezo ya kawaida ya barabara ya Ndogomi - Mnyooko & Matengenezo ya kawaida na Marekebisho ya sehemu korofi kwenye barabara ya Iyogwe - Chogoali.									
57048	Chakwale-Leshata	Idibo & Leshata	Idibo & Leshata						
57091	Leshata- Idibo	Idibo & Leshata	Idibo & Leshata						
57095	Ndogomi -Mnyooko	Madege	Chakwale-Madege, Ndogomi & Mnyooko	W/31	I	24/7/2018	6/8/2018	17/9/2018	115.00
57059	Iyogwe - Chogoali.	Iyogwe	Iyogwe, Kilama, Chogoali						
Matengenezo ya kawaida, Marekebisho ya sehemu korofi na Matengenezo ya muda maalum kwenye barabara ya Tabuhotel - Kitange & Marekebisho ya sehemu korofi kwenye barabara ya Kibedy - Shabiby S/S pamoja na Marekebisho ya sehemu korofi kwenye barabara ya Meshugi - Mnyunwe- Nagwai JCT.									
57012	Tabuhotel - Kitange	Chigela	Tabuhotel, Kitange Il, Iheneje, Idete, Kitangel						
57035	Kibedy - Shabiby S/S	Chigela	Mogohigwa, Kibedy	W/32	I	24/7/2018	6/8/2018	17/9/2018	104.25
Matengenezo ya kawaida ya barabara za Gairo Mjini & Matengenezo ya kawaida ya barabara ya Msingisi - Luhwaji pamoja na Matengenezo ya muda maalum kwenye barabara ya Ukwamani - Meshugi.									
57073	Halimashauri -Ukwamani	Magoweke	Ukwani						
57041	Msingisi - Luhwaji	Msingisi	Msingisi, Luhwaji	W/33	I	24/7/2018	6/8/2018	17/9/2018	95.50
	Ukwamani - Meshugi	Ukwamani & Mikala	Ukwamani, Mkalama & Meshugi4						